# TASAC yajivunia miaka miwili ya Rais Samia Suluhu Hassan

Na Mwandishi Wetu

SHIRIKA la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) lilianzishwa chini ya Kifungu cha 4 cha Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania, Sura ya 415 na kuanza rasmi kutekeleza majukumu yake Februari 23, 2018 kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 53 lilitolewa Februari 16, 2018.

Kuundwa kwa TASAC ni hatua ya kisera ya Serikali kwa upande wa Tanzania Bara, inayokusudia kukuza sekta za usafiri majini, kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma hususani kuchochea ukuaji wa uchumi wa Taifa kwa kuinua mchango wa usafiri kwa njia ya maji.

Hii ni kwa sababu Tanzania ina ukanda mkubwa wa Bahari ya Hindi wenye urefu takribani Kilomita 1,424, Maziwa makubwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa; hivyo kuwepo kwa fursa kubwa ya kukuza uchumi wa nchi yetu kupitia sekta hii, yaani uchumi wa rasilimali za maji (Blue Economy).

Aidha, TASAC inatekeleza majukumu ya udhibiti wa huduma za usafiri majini, usimamizi wa ulinzi na usalama wa usafiri majini na kuzuia uchafuzi wa mazingira utokanao na shughuli za usafiri majini, majukumu ambayo hapo awali yalikuwa chini ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA). Majukumu haya yalihamishwa kwenda TASAC kama ilivyoelekezwa katika Kifungu cha 68 cha Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania, Sura ya 415.



**Mkurugenzi Mkuu wa TASAC, Kaimu Abdi Mkeyenge, akifafanua jambo kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mashirika ya Umma (PAC).**

**MAJUKUMU YA TASAC**

Kwa mujibu wa Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania, Sura ya 415, majukumu makuu ya TASAC yapo kwenye vifungu vya 7, 11 na 12 kama ifuatavyo:

**(i) Kufanya kazi za Uwakala wa Forodha (Clearing & Forwarding Function) kwa bidhaa chache zenye maslahi mapana kwa Taifa.**

Bidhaa hizo ni pamoja na; Wanyama Pori kwa mujibu wa sheria ya usimamizi wa Wanyamapori, Kemikali zinazoagizwa na kutumika na kampuni za uchimbaji madini, Silaha za Moto na Vilipuzi, Nyara za Serikali na Makinikia.

**(ii) Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Usafiri Majini na Kuzuia Uchafuzi wa Mazingira utokanao na shughuli za usafiri majini (Maritime Administration).**

Katika kutekeleza majukumu haya, TASAC inasimamia yafuatayo:

- Utekelezaji wa Sheria ya Usalama wa Vyombo vya Majini, Sura ya 165 (The Merchant Shipping Act, Cap. 165);
- Utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa kuhusu Usafirishaji Majini inayoratibiwa na Shirika la Bahari Duniani (International Maritime Organization – IMO);
- Kufanya ukaguzi wa meli zilizosajiliwa nchini na meli za nje zinazoingia katika bandari za Tanzania Bara;
- Kudhibiti vivuko (Ferries);
- Kuratibu shughuli za utafutaji na uokoaji majini (Maritime Search and Rescue – SAR);
- Kudhibiti utunzaji wa mazingira dhidi ya uchafuzi utokanao na shughuli za meli; na
- Kutoa taarifa na uelewa kwa umma kuhusu masuala ya ulinzi, usalama na mazingira majini.

**(iii) Kudhibiti Watoa Huduma za Usafiri na Usafirishaji kwa njia ya maji nchini (Maritime Transport Regulation).**

Jukumu la udhibiti kwa Watoa Huduma za Usafiri na Usafirishaji kwa njia ya maji nchini linahusu Watoa Huduma za Bandari, Bandari Kavu, Upimaji wa Uzito wa Makasha (Gross Mass Verification – GMV), Uwakala wa Meli (Shipping Agency), Uwakala wa Forodha (Clearing and Forwarding Agency), Ukusanyaji na Utawanyaji wa Shehena (Cargo Consolidation and De-consolidation) na Udhibiti wa Watoa Huduma Mbalimbali Bandarini (Miscelaneous Port Services). Katika kutekeleza jukumu hili, TASAC inafanya kazi zifuatazo:

- Kutoa, kuhuisha au kufuta leseni za watoa huduma;
- Kusimamia utekelezaji wa viwango vya huduma zinazodhibitiwa;
- Kuweka na kusimamia masharti ya utoaji wa huduma zinazodhibitiwa;
- Kudhibiti tozo na ushindani miongoni mwa watoa huduma;
- Kufuatilia utendaji wa watoa huduma;
- Kuwezesha utatuzi wa malalamiko katika sekta inayodhibitiwa;
- Kusimamia mienendo ya watoa huduma katika sekta; na
- Kutoa taarifa kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu majukumu ya Shirika.

Kazi hizi zote zinafanywa kwa kuzingatia Sheria na Kanuni mahsusi kwa kila kundi la watoa huduma wanaodhibitiwa ili kukidhi matakwa ya aina tofauti za biashara kwenye sekta. Aidha, zipo Kanuni kwa ajili ya viwango vya huduma kwa watoa huduma wanaodhibitiwa, udhibiti wa tozo na Kanuni mahsusi kwa ajili ya utatuzi wa malalamiko kati ya watoa huduma na wateja wanaohudumiwa.

**MIRADI ILIYOTEKELEZWA NA TASAC KWA KIPINDI CHA MIAKA MIWILI YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA**

Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suhuhu Hassan,TASAC imetekeleza miradi mbalimbali ambapo miradi mingine bado inaendelea kutekelezwa kama ifuatavyo:

**(i) Mradi wa Uundaji wa Kanzidata ya Vyombo Vidogo vya Usafiri Majini Tanzania Bara**

TASAC kwa kushirikiana na wadau wengine ikiwemo Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Wizara ya Mifugo na Uvuvi na TAMISEMI ilifanya Sensa ya kwanza ya vyombo vidogo vya usafiri majini, ambapo taarifa kuhusu vyombo, umiliki na mahali vilipo nchini zilikusanywa na kuingizwa katika kanzidata kwa malengo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuboresha usimamizi wa usalama wa vyombo vya usafiri majini, utungaji wa sera na mipango itakayoongeza mchango wa uchumi wa rasilimali za maji katika pato la Taifa. Sensa ya namna hii ni ya kwanza kufanyika nchini.

**(ii) Mradi wa Kimataifa wa Mawasiliano na Uchukuzi katika Ziwa Victoria (Multi-National Lake Victoria Maritime Communication and Transport – MLVMCT)**

Ili kukuza uwekezaji katika shughuli za usafiri majini na uvuvi, Serikali ya Awamu ya Sita kupitia TASAC inaendelea kukamilisha Mradi wa Kimataifa wa Mawasiliano na Uchukuzi katika Ziwa Victoria (Multi-National Lake Victoria Maritime Communication and Transport – MLVMCT). Lengo la mradi huu ni kushughulikia changamoto za usafiri majini, kuimarisha usalama wa vyombo vya usafiri majini na kuongeza fursa za kiuchumi kwa jamii zinazoishi kandokando ya Ziwa Victoria.

Mradi huu unaotekelezwa na nchi za Tanzania na Uganda umepangwa kugharimu kiasi cha Shilingi Bilioni 59.23 ambapo upande wa Tanzania gharama za mradi ni Shilingi Bilioni 19.97 zinazojumuisha gharama za kazi za ndani na sehemu ya mchango wa Tanzania katika kugharamia kazi za kikanda zinazofanywa kwa kushirikiana na Uganda. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mnamo mwezi Disemba, 2024 na tayari Mshauri elekezi ameshakabidhiwa maeneo ya kufanyia kazi.

**(iii) Uendelezaji na Uimarishaji wa Miundombinu ya Mifumo ya TEHAMA**

TASAC inatekeleza miongozo inayotolewa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) katika kuhakikisha manunuzi, matumizi bora, sahihi na salama ya vifaa na mifumo yote ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) Serikalini. Katika kutekeleza hili, Shirika limeunganisha ofisi zake zote zikiwemo zile za Mikoa, Wilaya na mipaka kwenye Mkongo wa Taifa ambao umerahisisha na kuharakisha mawasiliano ya ndani (Intranet), barua pepe, na mawasiliano na wadau wa nje (Internet).

Uendelezaji miundombinu na mifumo ya TEHAMA ulianza mwaka wa fedha 2018/19 na utakamilika mwaka wa fedha 2025/26. Miundombinu na mifumo ya TEHAMA inayoboreshwa ndani ya Shirika ni pamoja na; mfumo wa ukaguzi, usajili wa vyombo vya usafiri kwa njia ya maji na utoaji wa vyeti vya Mabaharia (Maritime Administration Management System), mfumo wa utoaji leseni, ukusanyaji wa mapato ya udhibiti, uhakiki kadhia na kutoa ankara za malipo ya watoa huduma wa meli (Manifest Billing System), pamoja na mfumo wa kutoa huduma za biashara ya Meli (Shipping Business Management System – SBMS).

**MAFANIKIO**

Kwa kipindi cha miaka miwili ya Serikali ya Awamu ya Sita, TASAC inajivunia mambo mengi sana hususani juhudi za Serikali hii katika kuboresha sekta ya usafiri majini. Kati ya mafanikio ambayo TASAC inajivunia ni pamoja na:

**(i) Kuunda nyenzo za udhibiti wa huduma za usafiri majini**

Hii ni pamoja na kanuni na miongozo mbalimbali ambapo jumla ya kanuni mpya 11 chini ya Sheria ya Uwakala wa Meli, Sura 415 na kanuni nyingine 32 chini ya Sheria ya Usafiri Majini, Sura 165 zimeshaandaliwa na kuanza kutumika.

inaendelea ...UK 13



inatoka ...UK 12

# TASAC yajivunia miaka miwili ya Rais Samia Suluhu Hassan

**(iii) Kuwezesha ongezeko la idadi ya watoa huduma wanaodhibitiwa na TASAC**

Katika kutekeleza hili, idadi ya leseni na vyeti vya usajili ilifikia 1,195 kwa mwaka wa fedha 2021/22 ikilinganishwa na leseni na vyeti vya usajili 941 katika mwaka wa fedha 2018/19 sawa na ongezeko la asilimia 79.

Aidha, idadi ya vyeti vilivyotolewa kwa mabaharia waliokidhi masharti iliongezeka kutoka 6,068 katika mwaka 2018/19 hadi kufikia 19,575 katika mwaka 2021/22 sawa na ongezeko la asilimia 31.

**(iv) Kuimarisha udhibiti wa usalama na ulinzi**

TASAC imefanikiwa kurasimisha maeneo 20 ya kibandari katika mwambao wa bahari na maziwa.

**(v) Kusimamia utekelezaji wa mikataba, itifaki na miongozo inayotolewa na Shirika la Bahari Duniani**

TASAC inasimamia utekelezaji huo kwa niaba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaporidhia mikataba, itifaki na miongozo hiyo. Mpaka sasa TASAC inasimamia jumla ya mikataba sita ya kimataifa ya Shirika la Bahari Duniani (IMO) na kuendelea kufatilia uridhiaji wa mikataba mingine na mabadiliko yake ili kubadilisha sheria na kanuni za nchi katika sekta ya usafiri majini.

**(vi) Kuimarisha usimamizi wa usalama, ulinzi na utunzaji wa mazingira dhidi ya shughuli za meli**

Uimarishaji usimamizi, ulinzi na utunzaji wa mazingira unasaidia kupunguza matukio ya ajali za vyombo vya majini ambapo kaguzi za vyombo vya usafiri majini zilifanyika 6,208 katika mwaka wa fedha 2021/22 na kaguzi 4,490 katika kipindi cha Julai 2022 mpaka Januari 2023 inayotarajiwa kufikia vyombo takribani 8,000 ifikapo mwezi Juni 2023. Aidha, Shirika limekuwa likiratibu Mpango wa Taifa wa Kuzuia na Kupambana na Umwagikaji wa Mafuta Baharini.

**(vii) Kuimarisha Usimamiaji na utoaji wa vyeti vya Mabaharia kwa kuzingatia matakwa ya Shirika la Bahari Duniani (IMO)**

Chini ya mkataba wa STCW 1978, TASAC kwa niaba ya Serikali ya Tanzania, imeimarisha usimamizi wa utoaji wav yeti vya mabaharia kwa kuzingatia Shirika la Bahari Dunia (IMO) ambapo kwa mwaka wa fedha 2021/22 vyeti 16,718 vilitolewa. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2022 mpaka Januari 2023, Shirika liliweza kutoa vyeti 9,570 vinavyotarajiwa kufikia vyeti takribani 1,700 ifikapo Juni 2023.

**(viii) Kuongeza mchango katika Mfuko Mkuu wa Serikali**

TASAC imefanikiwa kuongeza mchango katika Mfuko Mkuu wa Serikali mwaka hadi mwaka kutoka Shilingi Bilioni 9.1 katika mwaka wa fedha 2018/19 hadi kufikia Shilingi Bilioni 43.5 katika mwaka wa fedha 2021/22 sawa na ongezeko la asilimia 21 na hivyo kufanya jumla ya mchango wa TASAC katika mfuko mkuu wa Serikali kwa kipindi cha miaka minne kuwa Shilingi Bilioni 104.5.

**(ix) Kupata Hati Safi za Ukaguzi wa Hesabu (Unqualified Opinion)**

TASAC imefanikiwa kupata hati safi za Ukaguzi wa Hesabu kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa miaka mitatu mfululizo tangu ilipoanza kutekeleza majukumu yake mwaka 2018. Hati safi hizi zilipatikana katika miaka ya fedha ya 2018/19, 2019/20 na 2020/21 mtawalia.

**(x) Kuimarisha utoaji wa huduma kwa kiwango cha kimataifa**

Shirika limeweza kuimarisha utoaji wa huduma kwa kiwango cha kimataifa na kufikia mahitaji ya wateja na hata matarajio zaidi na hivyo kuwezesha kupata cheti cha ubora cha mfumo wa usimamizi wa ubora ISO 9001: 2015.

**(xi) Kusimamia vizuri viwango vya ubora wa huduma za bandari na meli**

Katka kipindi hicho TASAC imeweza kusimamia vizuri viwango vya ubora wa huduma za bandari na meli, hivyo kuongeza kuridhika kwa wateja na kuzifanya bandari zetu kuaminika na wateja wa ndani na nje ya nchi.

**(xii) Kuboresha ufanisi wa bandari kwa kupunguza uwezo wa shehena inayoruhusiwa**

TASAC imefanikiwa kuboresha ufanisi wa bandari kwa kupunguza uwezo wa shehena inayoruhusiwa kukaa bandarini kwa wakati mmoja (yard density) kutoka asilimia 65 hadi asilimia 50 kwa kuweka Amri ya Tozo ya Bandari Kavu.

**(xiii) Kufungua ofisi 11 za Shirika katika maeneo mbalimbali**

Katika kipindi hicho, TASAC imeweza kufungua ofisi 11 katika maeneo mbalimbali nchini ili kusogeza huduma karibu na wananchi. Kwa sasa Shirika lina ofisi katika maeneo yafuatayo; Dar es Salaam, Dodoma, Mtwara, Tanga, Mwanza, Kagera, Mara, Kigoma, Rukwa, Ukerewe na Geita.

**(xiv) Kushirikiana na Shirika la Bahari Duniani (IMO) katika kuratibu mafunzo ya kikanda**

TASAC ilishirikiana kwa karibu na IMO kuratibu mafunzo ya kikanda ambapo nchi 15 za kanda ya Afrika zilishiriki mafunzo ya jinsi ya kukabiliana na maji yanayotumika kuweka uwiano melini yaani "Ballast Water Management" ambayo yalifanyika mwezi Disemba, 2022 jijini Dar es Salaam na Mwezi huu wa tatu watakuja kutoa mafunzo kwa wakufunzi wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) kuhusu masuala hayo ya "Ballast Water Management".

**(xv) Kuimarisha ushirikiano na Mamlaka ya Bahari Zanzibar (ZMA)**

Katika kipindi hicho, TASAC imeimarisha ushirikiano na Mamlaka ya Bandari Zanzibar kwa kuwa na kaguzi za pamoja kwa vyombo vya usafiri majini, utoaji elimu ya usalama majini, utafutaji na uokoaji.

**(xvi) Kutekeleza kwa zaidi ya asilimia 70 ya mapendekezo kutokana na hoja za ukaguzi uliofanywa na IMO**

TASAC ilifanikiwa kutekeleza kwa zaidi ya 70% mapendekezo kutokana na hoja zilizotolewa na Shirika la Bahari Duniani (IMO Member State Audit Scheme -IMSAS) nchini Tanzania, mwaka 2019.

**(xvii) Kufanya mapitio ya tozo mbalimbali**

Katika kipindi hicho TASAC ilifanya mapitio ya tozo mbalimbali na kuzifuta tozo ambazo zilibainika kuwa hazina msingi wa kuendelea kuwepo.

**(xviii) Kutwaa ushindi katika mashindano ya uandaaji wa hesabu**

TASAC ilifanikiwa kunyakua tuzo ya ushindi katika mashindano ya uandaaji wa hesabu za fedha za Mwaka 2020/21 kwenye kundi la mamlaka za udhibiti.

(xix) Kuwa miongoni mwa taasisi kumi bora Tanzania

TASAC pia ilifanikiwa kuwa miongoni mwa taasisi 10 bora Tanzania katika mwaka wa fedha 2020/21 kufuatia ukaguzi uliofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA);

**(xx) Kukagua meli za nje zinazofika katika bandari zetu**

TASAC iliweza kukagua meli za nje zinazofika katika bandari zetu kwa mujibu wa Makubaliano ya nchi zinazopakana na Bahari ya Hindi (Indian Ocean Memorandum of Understanding – IOMOU) ambayo Tanzania ni mwanachama.

**(xxi) Kuanzisha majadiliano ya kuingia katika makubaliano (Memorandum of Understanding – MoUs) ya kutambuliana vyeti vya mabaharia**

Katika kipindi hicho, TASAC ilianzisha majadiliano ya kuingia katika makubaliano ya kutambuliana vyeti vya maharia ili kufungua fursa za ajira kwa mabaharia wetu na nchi 19 ikiwemo Panama, Malta, Cyprus; Ghana pamoja na Jamhuri ya Watu wa China.

**(xxii) Kuwajengea uwezo maafisa 42 kutoka taasisi mbalimbali za Serikali**

TASAC ilifanikiwa kuwajengea uwezo maafisa 42 kutoka taasisi mbalimbali za Serikali kuhusu uratibu wa utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Dharura wa kukabiliana na umwagikaji wa mafuta baharini (National Maritime Oil Spill Response Contingency Plan – NMOSRCP).

**(xxiii) Kufanya Sensa ya kwanza ya vyombo vidogo vya usafiri majini**

TASAC ilifanya sense ya kwanza ya vyombo vidogo vya usafiri majini vinavyotumika katika usafirishaji wa abiria, mizigo na uvuvi katika maeneo yote yenye maji ikiwemo bahari, maziwa, mito na mabwawa kwa Tanzania Bara; na

**(xxiv) Kuongeza utoaji wa elimu ya usalama wa usafiri majini kwa umma**

Katika kipindi hicho, TASAC iliweza kuongeza kasi ya utoaji elimu ya usalama wa usafiri majini kwa umma kwa kuongeza idadi ya mikutano ya usalama katika maeneo mbalimbali.

**FURSA ZILIZOPO KATIKA SEKTA YA USAFIRI MAJINI**

Mbali na Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho lakini pia kuna fursa mbalimbali katika Sekta ya Usafiri Majini ambazo zinaweza kukuza uchumi na kuongeza ajira kwa wananchi kama vile; kuanzisha usajili wa meli kwa masharti nafuu, kuanzisha maeneo ya ukarabati na ujenzi wa meli katika ukanda wa pwani; kuanzisha maegesho ya boti ndogo katika ukanda wa pwani, kuanzisha viwanda vya utengenezaji malighafi za ujenzi wa boti za plastiki pamoja na kujenga bandari rasmi za uvuvi.

**HITIMISHO**

TASAC inaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa ikiwemo kusimamia Mradi wa Kimataifa wa Mawasiliano na Uchukuzi katika Ziwa Victoria (Multi-National Lake Victoria Maritime Communication and Transport – MLVMCT).

Pia inaishukuru Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi chini ya Mhe. Prof. Makame Mbarawa, kwa kuendelea kutusimamia na kutuongoza vyema katika utekelezaji wa majukumu yetu.



**Baadhi ya makasha yakiwa kwenye meli kabla ya kushushwa bandarini**